JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA


| | | |
|---|---|---|
| SIMU: 027-2756366<br>FAX: 027-2756521<br>E-mail: marangutc@moe.go.tz<br>Unapojibu tafadhali taja: | | Chuo Cha Ualimu Marangu,<br>S.L.P. 266,<br>MARANGU,<br>KILIMANJARO. |


| | | |
|---|---|---|
| Kumb.Na.MTC/MKV/03/VOL.IV/52 | | 04 Juni , 2026 |

Ndugu …………………………………

S.L. P …………………………………...

……………………………………….

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STAHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI KWA PROGRAMU YA KAWAIDA NA ELIMU MASAFA KWA MWAKA WA MASOMO 2026-2027 KATIKA CHUO CHA UALIMU MARANGU

1. (a) Utangulizi

Uongozi na jumuiya yote ya Chuo Cha Ualimu Marangu wanakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu katika Chuo hiki. Hongera sana! Chuo hiki kinaendesha mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi kwa programu mbili; programu ya kawaida na programu ya elimu kwa njia ya masafa. Progamu ya Ualimu Kwa Njia ya Kawaida ni ya miaka miwili na walengwa katika programu hii ni Wahitimu wa Kidato Cha Sita, na walimu ambao walishahitimu Astashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi. Programu ya Elimu Kwa Njia ya Masafa ni ya miaka mitatu mpaka minne na inawalenga walimu wenye Astashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi.

Wanachuo watakaokuwa wamechaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu kwa programu ya kawaida kwa mwaka wa masomo, 2026-2027, wanatakiwa kuripoti chuoni kuanzia tarehe 18-08-2026; na mwisho wa kuripoti itakuwa ni tarehe 03 -09-2026. Wanachuo watakaokuwa wamechaguliwa kwa programu ya ualimu kwa njia ya masafa watapewa maelekezo ya muda wa kuanza mafunzo baadaye.

b) Mahali Chuo Kilipo na Usafiri wa Kukufikisha Chuoni:

Chuo hiki kipo katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Moshi Vijijini, eneo la Marangu, umbali wa kilometa moja kutoka stendi ya mabasi Marangu Mtoni katika barabara kuu ya kuelekea Rombo na pacha ya kwenda Kinapa (Kilimanjaro National Park). Kuna usafiri wa mabasi (daladala) kutoka Moshi Mjini ambayo pia yanapita njiapanda itokayo Dar-es-salaam; mahali ambapo wale watokao njia ya Dar es Salaam wanaweza kuteremkia na kupanda mabasi ya kuja Marangu moja kwa

moja bila kufika Moshi Mjini. Mahali pa kuteremkia panaitwa Njia Panda ya Himo. Mabasi yanayoweza kukufikisha chuoni ni yale yaendayo Marangu Mtoni, Mwika na Kilema. Ukipanda ya Marangu Mtoni na Mwika teremkia Marangu Mtoni. Ukipanda ya Kilema teremkia kwenye lango la kuingilia (getini) chuoni, Chuo cha Ualimu Marangu. Kwa wale wanatokea Dar-es-salaam au Dodoma, mabasi yanayoweza kukufikisha chuoni ni yale yaendayo Rombo. Ukipanda mabasi hayo teremkia Marangu Mtoni.

c) Dira na Moto wa Chuo

- Dhima ya Chuo: Kuandaa walimu bora watakaohimili ushindani wa soko la ajira kwa kutumia mbinu bora na za kisasa za ufundishaji.
- Dira: Kuwa kituo cha kutoa walimu mahiri katika viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Moto wa Chuo: Elimu ni Kazi.

2: Mahitaji Kwaajili ya Usajili

a) Vyeti na Hati za Utambulisho:

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uje na vyeti halisi (Original) halali vifuatavyo:-

i. Vyeti vya Taaluma (Academic Certificates) vya kidato cha Nne (IV) na Sita (VI); Astashahada ya Ualimu (Ualimu Daraja A) au Hati ya Matokeo (Result Slip) kwa ambao vyeti vyao havijatolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Kama umefanya mitihani zaidi ya mara moja, uje na vyeti vyote.
ii. Vyeti vya kuhitimu (Leaving certificates) vya shule uliyosomea.
iii. Cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)
iv. Hati yoyote ya ziada inayoweza kusaidia kukutambulisha na kuthibitisha uhalali wako na uhalali wa umiliki wa nyaraka zako za kitaaluma na kitaalamu; mfano NIDA.
v. Barua ya ruhusa ya mwajiri kwa walioajiriwa.

b) Ada: Kwa wanachuo wa programu ya kawaida; ada ya mafunzo kwa mwaka ni shilingi 450,000/=. Unaweza kulipa yote au ukalipa shilingi 225,000/= kwa muhula. Kabla ya kufanya malipo ya fedha hizi wasilianana na watendaji wa ofisi ya usajili ili upewe namba ya kudhibiti malipo (control number) ya fedha hiyo. Namba za watendaji wa Ofisi ya Usajili ni (1) Dkt. Joyce Mchilo 0712238491, 0769355291 (2). James Kitalala 0683162801, 0757159365 (3). Febronia Kereti 0764715733, 0785438318.

c) Michango: Kwa wanachuo wa programu ya kawaida; Mbali na ada kila mwombaji wa mafunzo aliyechaguliwa ili asajiliwe anatakiwa kulipa michango ifuatayo:

| Na | MCHANGO | KIASI | UFAFANUZI |
|---|---|---|---|
| | Serikali ya Wanachuo | 5,000.00 | Kwa Mwaka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | Huduma ya Kwanza | 10,000.00 | Kwa Mwaka |
| 3. | Usafi na Mazingira | 20,000.00 | Kwa Mwaka |
| 4. | Kukodisha Godoro | 10,000.00 | Kwa Mwaka |
| 5. | Usajili na Kitambulisho | 20,000.00 | Mara Moja |
| 6. | Michezo | 30,000.00 | Kwa Mwaka |
| 7. | Ulinzi | 30,000.00 | Kwa Mwaka |
| 8. | Ukarabati wa Miundo Mbinu | 25,000.00 | Kwa Mwaka |
| 9. | Bima ya Afya | 50,400.00 | Kwa Mwaka |
| 10. | T.Shirt | 20, 000.00 | Mara Moja. |
| | Jumla | 220, 400.00 | |

Aidha, malipo ya michango yote, kuanzia namba 1 mpaka 10 hapo juu, yalipwe kwenye Benki ya NMB, A/C no. 40301100014: Jina la akaunti Marangu Teachers' College Education Development. Malipo haya yanatakiwa kufanyika mara moja unapoanza chuo.

N.B. Kwa malipo yote ya ada na michango utakayofanya benki au kwa wakala hakikisha una hati ya kuingizia pesa hizo (bank pay in slip) ambayo utakuja nayo chuoni ili upewe risiti ya malipo uliyoyafanya. Pia ni muhimu sana kwa mzazi au mwanachuo mwenyewe anayefanya malipo, kuhakikisha kuwa hati hiyo ya kuwekea pesa (pay in slip) imeandikwa jina la mwanachuo anayelifanyiwa malipo. Kwa wanachuo watakaochaguliwa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu, Elimu ya Msingi Kwa Njia ya Elimu Masafa watapaswa Kulipa ada ya Shilingi 450,000.00 na Michango Shilingi 150,000.00 Kwa Mwaka.

d) Sare Kwa Wanachuo wa Programu ya Kawaida ya Miaka Miwili.

1. Sare ya Chuo: Wasichana: Jozi mbili: Shati la mikono mirefu rangi ya bluu bahari (light blue), Suti ya koti la mikono mirefu na sketi, vya rangi ya dark blue. Sketi iwe ya mshono wa suti yenye pindo moja tu mbele, urefu wa kutosha (iwe ya heshima isiyo ya kubana) na tai ya dark blue inayofanana na suti. Kitambaa cheusi cha kichwani (Hijab Nyeusi) Kwa Waislamu.
2. Sare ya Chuo: Wanaume: Jozi mbili: Shati la mikono mirefu rangi ya bluu bahari (light blue), suti ya koti la mikono mirefu, tai rangi ya "dark blue" inayofanana na suti pamoja na suruali vya rangi ya dark blue". Suruali iwe na luksi kwaajili ya kufungia mkanda, marinda mawili kila upande. Pia iwe na mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma wenye kifungo. Chini iwe na upana kati ya inchi 15 na 18; na urefu wa kutosha kufikia viatu.
3. Sare ya Chuo Kwa Wanachuo wa Programu ya Kawaida: Wote: T. Shirt Yenye Nembo ya Chuo. Kila Mwanachuo atakayesajiliwa atatakiwa kulipia shilingi 20,000.00 kwaajili ya sare ya T-shirt itakayotolewa chuoni.

4. Sare ya Chuo: Wanachuo wa Programu ya Kawaida. Wote: Viatu: Viatu

vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu, visiwe na visigino virefu, jozi mbili, soksi nyeupe kwa wasichana na bluu/ nyeusi kwa wanaume.

N.B: Utatakiwa kuvaa sare ya chuo na mavazi NADHIFU na ya HESHIMA yatakayoendana na maadili ya Ualimu wakati wote. Sare ya chuo isiwe ya mtumba. Utaratibu wa kuvaa T-Shirt yenye nembo ya chuo kama sare utatolewa chuoni.

Tanbihi: Kama unapata shida ya kubainisha rangi na mshono halisi, nguo hizi unaweza ukashona katika maeneo ya karibu na chuo baada ya kufika chuoni.

e) Mavazi ya Michezo: Wanachuo wa Programu ya Kawaida - (i) Wahitimu wa Kidato Cha 6: Track suit rangi ya bluu / dark blue (ii). Wahitimu wa Astashahada ya Ualimu: Track suit rangi ya kijivu. (iii) Raba nyeusi/bluu kwa wote; wahitimu wa kidato cha 6 na Astashahada ya Ualimu.

f) Mahitaji ya Nguo kwa ajili ya Malazi: Wanachuo wa Programu ya Kawaida. Shuka mbili rangi ya light blue wanaume, pink wanawake, bed cover nyeupe, mto na foronya, chandarua ya kuzuia mbu, blanketi, sweta ya shingo ndefu –pullneck ya rangi nyeusi au darkblue (matumizi wakati wa baridi); Marangu kuna baridi. Pia utatakiwa kuwa na pazia kubwa zito la rangi nyeupe lenye upana wa mita mbili na nusu kwa ajili ya dirisha la chumba utakachokuwa unalala.

3. Mahitaji ya Taaluma: Wanachuo wa programu ya Kawaida.

- Daftari zisizopungua 12 aina ya 'counter book' za 2 'quires,'
- Kalamu za kuandikia,
- Mafaili ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali za kitaaluma,
- Bunda moja ya Karatasi za Photocopy A-4.

Wanachuo wa programu ya Stashahda ya Ualimu, Elimu ya Msingi Kwa Njia ya Masafa watapewa maelekezo wakati wa mafunzo kabilishi.

4. Afya:

(a) Ili uweze kukubaliwa kusomea Mafunzo ya Ualimu unahitajika kupimwa afya yako na kuthibitishwa na Daktari anayetambulika kisheria kwa kujaza fomu (Request for Medical Examination) iliyoambatanishwa ambayo utakuja nayo chuoni. Hakikisha kuwa fomu hiyo imepigwa muhuri wa Ofisi ya Daktari wa Hospitali inayotambulika kisheria.

(b) Kwa kupitia Mchango wa Matibabu utakaotoa unapojiunga, na baadaye kila mwaka, Chuo kitatoa huduma ya kwanza katika zahanati ya chuo.

(c) Kupitia mchango wa Bima endapo utahitaji huduma ya zaidi ya Huduma ya kwanza inayotolewa Chuoni; utaenda kupata matibabu nje ya chuo. Kama una kadi ya bima ya afya uje nayo na hivyo hutahitaji kulipia Bima ya Afya ya shilingi 50,400/= iliyotajwa awali kwenye Jedwali la michango.

5. Mahitaji Mengine.

Mahitaji mengine madogomadogo kama vifaa vya usafi binafsi, vyombo vya

chakula na kadhalika utajinunulia mwenyewe ufikapo chuoni baada ya kupewa maelekezo. Hakikisha una fedha za kutosha kukidhi mahitaji yako binafsi.

6. Kanuni na Taratibu Nyingine.
Ufikapo chuoni utapewa kanuni na taratibu zinazoongoza mwenendo na mahitaji ya mafunzo ya ualimu. Miongozo hiyo ya kanuni, taratibu na sheria za chuo imewekwa ili kuhakikisha kuwa viwango vya utendaji kitaaluma na mwenendo wa mwanachuo kwa ujumla vinakidhi vigezo vya mafunzo ya ualimu. Kwa ujumla wake taratibu na kanuni za Mafunzo ya Ualimu haziruhusu unywaji wa pombe, ulevi wa aina yoyote ile na tabia zote zisizo za kimaadili. Baada ya kusoma kanuni na sheria za chuo utapewa fomu ya kujaza ili kuridhia kabla ya kusajiliwa. Kujisajili maana yake ni kuridhia kuzifuata wakati wote utakapokuwa chuoni.

7. Mawasiliano:
Endapo utakwama na kuhitaji msaada au ufafanuzi zaidi wasiliana na watendaji wafuatao wa Ofisi ya Usajili .

- (1) Dkt. Joyce Mchilo 0769355291; 0712238491. (2) James Kitalala 0683162801; 0757159365 (3). Febronia Kereti 0785438318; 0764715733.

Aidha taarifa zote muhimu zinazomhusu mwanachuo anapokuwa chuoni mfano maafa, msiba, ugonjwa toka nyumbani lazima zipitie kwa Mkuu wa Chuo na siyo kwa mwanachuo moja kwa moja. Wazazi/Walezi/Ndugu/ Waajiri wanapaswa kuzingatia utaratibu huu wa mawasiliano kwa ajili ya usalama na uratibu wa masuala ya wanachuo.

8. Mwisho:

Kumbuka kuwa siku zote mwalimu anapaswa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa mazuri na wanafunzi wake na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo kila mwanachuo

anatazamiwa awe na tabia nzuri na **mwenendo unaoakisi maadili ya ki-ualimu** wakati wote wa mafunzo yake na baada ya mafunzo hayo.

**TUNAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA YA KUJA CHUONI.**

**KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU MARANGU.**

……………………………….

**Dkt. CHAMBULILA, G.D**

**MKUU WA CHUO**

| | | |
|---|---|---|
| | | From: The Principal,<br>MaranguTeachers'College,<br>P.O. Box 266,<br>MARANGU. |

PART A

To the Medical Officer.

…………………………………………….

REF: MR/MRS/MISS ……………………………………………………………………

(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course. The examination should include the following categories (I-III). Each category of which will render the applicant in-eligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate in eligible for the course, including category V:

I. (a) Eye Sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e) Venereal Disease
(f) Leprosy
(g) Peptic Ulcers
(h) Epilepsy
(i) Tuberculosis
II. Neuroses
III. Other Serious Diseases
IV. Pregnancy
V. Mental and Physical Fitness

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/un fit for a full time teacher training course.

1. (a) Eye Sight ……………………………. (f) Leprosy ……………………..
(b) Hearing ……………………………. (g) Peptic Ulcers ………………..
(c) Speech ……………………………….. (h) Epilepsy ………………………
(d) Limbs ………….. ………………….. (i) Tuberculosis …………………..
(e) Venereal Disease ……………………..
II. Neuroses ……………………………………………………….
III. Other Serious Diseases ……………………………………..
IV. Pregnancy ……………………………………………………..
V. Mental and Physical Fitness ………………………………….
Date ……………………. Signature and official stamp ……………………….

Station ........................... Designation ..................................................